

## **USIMAMIZI BORA WA MIRATHI KWA MAENDELEO YA FAMILIA**

Uzoefu unaonesha kuwa, matatizo mengi hujitokeza katika familia au koo pale mtu anapofariki. Matatizo hayo hutokana na kutokujua taratibu za kusimamia na kugawa mali za marehemu kwa warithi wanaotambulika kisheria.

Mirathi ni taratibu za kisheria zinazoongoza ukusanyaji, uangalizi, usimamizi na hatimaye ugawaji wa mali za marehemu kwa wahusika. Taratibu hizi hutoa muongozo kama marehemu alifariki pasipo kuacha wosia au kwa kuacha wosia.

Mgawanyo wa mirathi nchini unategemea na mwenendo wa maisha ya marehemu kabla ya kifo chake. Hii inasaidia kuamua ni Sheria gani itumike katika kushughulikia mali zake. Sheria zinazosimamia utaratibu wa urithi na mirathi ni kama zifuatazo:

- a. Sheria ya Kiserikali
- b. Sheria ya Kiislamu
- c. Sheria ya Kimila

Sheria hizi zitamuongoza mtu yejote anayehitaji kuandaa wosia, ili ajue kutokana na imani au hadhi yake ni taratibu za sheria ipi atapaswa kutumia katika kuandaa wosia wake, au sheria ipi itawaongoza wanafamilia au wanaukoo wa marehemu katika ugawanywaji wa mali za marehemu ikitokea marehemu amefariki pasipo kuacha wosia.

Itambulike kuwa, kuna aina mbili za wosia, yaani wosia wa maandishi na wosia wa mdomo. Sheria za Usimamizi wa Mirathi zimetoa vigezo vya uandaaji wa aina hizi mbili za wosia. Lengo kuu la uwepo wa Sheria za usimamizi wa Mirathi ni kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba mali na madeni ya marehemu yanasmamiwa kwa namna ambayo inazuia uwezekano wa kuhatarisha amani au kusababisha madhara kwa warithi wa marehemu au kwa wadeni wake.

Vilevile katika kulinda na kutunza mali za marehemu ni lazima shauri la mirathi lifunguliwe na Msimamizi wa mirathi mahakamani ili kuweza kupata barua ya usimamizi wa mirathi. Si halali kugawanya au kuuza mali ya marehemu bila kufuata utaratibu huu.

Shauri la mirathi linaweza funguliwa katika mahakama mbalimbali, hii hutegemea na sheria itakayosimamia mirathi husika kama;

- a. Shauri la mirathi linalohusu Sheria za Kimila au Sheria ya Kiislamu litafuguliwa Mahakama ya Mwanzo.
- b. Shauri la mirathi linalohusu Sheria za Kiserikali linashughulikiwa au kufunguliwa katika Mahakama ya Wilaya/ Hakimu Mkazi na Mahakama kuu.

Familia ya marehemu inapaswa kusajili kifo ndani ya siku 30 katika ofisi ya vizazi na vifo, na endapo marehemu amefariki pasipo kuacha wosia familia ya marehemu au koo itapaswa kufanya kikao na kumchagua msimamizi wa mirathi, ambaye atafungua shauri la mirathi

katika mahakama husika. Kama hakutakuwa na pingamizi lolote mahakama itatoa barua ya usimamizi wa mirathi kwa Msimamizi wa Mirathi ambaye atapaswa kukusanya, kusimamia na kugawanya mali za marehemu ndani ya miezi sita kwa warithi wanaotambulika kisheria, na mwisho kuwasilisha mahakamani hati inayoorodhesha mali na jinsi zilivyogawanywa katika mahakama aliyofungulia shauri la mirathi hilo.

Taratibu za ufuutiliaji wa shauri la mirathi zinaweza zikachakua muda, hivyo katika kulinda, kuendeleza na kusimamia mali za marehemu, Sheria za mirathi pia zinatoa utaratibu wa jinsi ya kutunza au kusimamia mirathi ya marehemu hata kabla ya kutolewa barua ya usimamizi wa mirathi kwa kumchagua msimamizi wa mirathi wa muda ambaye ana lengo zuri na mali za marehemu.

Usimamizi bora wa mirathi unazingatia taratibu zote zilizoainishwa kisheria, hatahivyo watu wanapaswa kuondoa dhana potofu iliyopo katika kuandaa wosia mapema, maana wosia husaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza migogoro ya mirathi katika familia.

**Kumbuka;**

“Kutokujua Sheria hakuwezi kumwondelea hatia mtuhumiwa”

Kwa maswali au ufanuzi zaidi juu ya Sheria za Usimamizi wa Mirathi au swala lolote lile la kisheria, usisite kuwasiliana nasi kwa njia ya website [www.sheriakiganjani.co.tz](http://www.sheriakiganjani.co.tz) au kwa namba ya simu +255621900555.